

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA LUDEWA**



www.ludewadc.go.tz

KONGAMANO LA 9 LA BIASHARA ZANZIBAR

Januari 03, 2023

ZANZIBAR, TANZANIA

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa Mhe. Wise Mgina leo Januari 03, 2023 ameungana na Watanzania na wasio Watanzania kushiriki kongamano la 9 la biashara linalotarajiwa kufunguliwa rasmi kesho January 04 mwaka huu katika uwanja wa Maisala Mjini Magharibi Zanzibar.

Mhe. Wise Mgina ameongozana na wataalamu mbalimbali kutoka Wilayani Ludewa akiwemo Mkuu wa Disheni ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji Bi. Anusiata Mapunda, Afisa biashara Bw. Nicco Mchilo, Afisa Habari wa Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa Ndg. Chrispin Kalinga, Afisa Utalii wa Wilaya ya Ludewa Andrew Njavike pamoja na Wajasiliamali na wabunifu akiwemo mzee Reuben Mtitu maarufu kama Kisangani.

Wilaya ya Ludewa ilipata Mwaliko wa kushiriki Kongamano hilo ili Kuhamasisha Uwekezaji katika sekta ya Utalii, Kilimo, Uvuvi na Madini.

Pamoja na mambo mengine, viongozi hao wa Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa wamepata nafasi ya kukutana na viongozi mbalimbali wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na kuzungumza na kupeana elimu ya namna ya kuboresha na kuanzisha vyanzo vipya vya utalii kwa faida ya Halmashauri na Taifa kwa ujumla.

Chrispin B. Kalinga

Afisa Habari na Mawasiliano Serikalini

Ludewa ya Utalii, Uchumi wa Chuma na Maka ya Mawe kwa Maendeleo Yetu.